

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



OFISI YA RAIS,
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA



HALMASHAURI YA JIJI LA DAR ES SALAAM

Tarehe: 26 Januari, 2021

TANGAZO LA NAFASI YA KAZI YA KUKUSANYA USHURU WA MAEGESHO YA MAGARI MAENEO RASMI NA YASIYO RASMI (WRONG PARKING) WILAYA YA TEMEKE, ILALA NA KINONDONI, USHURU WA MLANGONI NA VYOONI KITUO KIKUU CHA MABASI UBUNGO/MBEZI LUIS, USHURU WA VYOO NA USAFI KATIKA MAENEO YA HALMASHAURI YA JIJI YA DAR ES SALAAM

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam anawatangazia wakazi wa Jiji la Dar es Salaam wenye sifa, nafasi ya kazi ya kukusanya ushuru wa maegesho ya magari maeneo rasmi na yasiyo rasmi (Wrong Parking), ushuru wa milangoni kituo kikuu cha mabasi Ubungo/Mbezi Luis na vyooni na usafi katika maeneo ya Mamlaka ya Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam. Kazi hii itakuwa ni ya Mkataba wa miezi mitatu na mshahara utalipwa kwa kuzingatia Sheria ya Ajira Cap. 300 "Wage Order" 2013 ambao utalipwa kuanzia shilingi laki moja na elfu hamsini (150,000.00) kwa mwezi.

SIFA ZA MWOMBAJI

- Awe raia wa Tanzania mwenye umri usiopungua miaka 18 na umri usiozidi miaka 60
- Awe na uwezo wa kutumia simu janja "Smartphone" katika miamala ya malipo
- Awe na uzoefu usiopungua miezi sita katika masuala ya kukusanya ushuru na usafi
- Awe mwadilifu na mwaminifu na awe hajawahi kutiwa hatiani kwa kosa la jinai.
- Awe na elimu kuanzia darasa la saba na kuendelea (**Wenye elimu ya kidato cha nne watapewa kipaumbele**).

MAELEKEZO YA JUMLA

- Waombaji waambatishe vivuli vya vyeti vya taaluma zao pamoja na cheti cha kuzaliwa.
- Kila barua ya muombaji iambatishwe na picha mbili ndogo (Passport size) iliyopigwa siku za karibuni, anuani kamili ya makazi pamoja na namba ya simu.

- **Barua ya maombi iambatishwe na:**

- ~ Barua kutoka kwa wadhamini wawili ambao ni watumishi wa Serikali zikiwa na picha "Passportsize" ya hivi karibuni, anuani kamili ya makazi, pamoja na namba zao za simu.
- ~ Barua ya utambulisho kutoka kwa Mwenyekiti wa Serikali za Mitaa.
- ~ Wasifu (CV).
- ~ Barua ya maombi ya kazi iletwe kwa njia ya mkono katika Ofisi ya Mkurugenzi wa Jiji la Dar es Salaam kuanzia tarehe ya tangazo hili au kwa njia ya posta kupitia anuani tajwa hapo chini kuanzia saa mbili kamili (2:00) asubuhi na mwisho wa kupokea barua ni tarehe 05 Februari, 2021 saa 8:00 mchana.

Kila mwombaji anapaswa kutaja nafasi ya kazi anayoomba juu ya bahasha ya maombi.

Maombi yatumwe kwa Anuani ifuatayo:-

Mkurugenzi wa Jiji,
Halmashauri ya Jiji,
Ukumbi wa Jiji,
1 Barabara ya Morogoro,
S.L.P. 9084,
11882 – DAR ES SALAAM

Tangazo hili pia linapatikana kwenye tovuti ya Halmashauri ya Jiji la Dar es salaam ambayo ni www.dcc.go.tz



Sipora J. Liana
MKURUGENZI WA JIJI